Kwa Watunzi na walimu wa shule au jamii iliyo na watoto wenye ualbino:

Kutoka: Every Child Ministries (Huduma ya Kila Mtoto)
Huduma ya Kikristo isiyo ya kiserikali inayoleta tumaini “Kwa watoto wa Afrika waliosahaulika”
Kwasababu WATOTO ni rasilimali kubwa zaidi ya nchi yoyote –
Hazina ya thamani kutoka kwa Mungu!

Every Child Ministries Uganda (Huduma ya Kila Mtoto Uganda)
PO Box 28080 Kampala

Kwa Watunzi wa shule na walimu,

Salamu kutoka kwetu! Tunashukuru kwa kujitolea kwenu kwa kutumikia taifa la Uganda na hasa kwa kuimarisha tabia ya vijana kupitia elimu. Mmechagua kazi yenye changamoto nyingi. Mungu awabariki kwa kuwaongezea nguvu na hekima.

Madhumuni ya kuwaandikia barua hii ni kwa sababu shule yenu ina mtoto aliye na ualbino, ambayo ni hali ya kimaumbile ambayo madhara yake ni pamoja na kutoona vizuri na huweza kusababisha saratani ya ngozi kama ngozi ya mtoto huyo imewekwa wazi kwa madhara ya jua.

Watoto walio na ualbino wanayo uwezo wa kiakili wa kawaida, na hujengeka kikawaida, na huchangia katika kuimarisha jamii, nao huishi upana wa maisha ya kawaida lakini kwa kutumia tahadhari kiasi.

Mnayo uwezo wa kuimarisha maisha ya watoto hawa kwa njia kadhaa, na tunawaomba mtumie nafasi zenu za mamlaka mliobarikiwa na Mungu ili kuleta ushawishi wa manufaa kwao.

Mwaweza kusaidia kwa:

- Kuhakikisha kuwa watoto wenye ualbino wameketi ambapo wanaweza kuona ubao vizuri. Tafadhali waruhusu kufanya majaribio kwa kukaa karibu na ubao ili kuona kama yaweza kuwasaidia.

- Kutumia chapa au matumizi ya viongezi vya kushikwa kwa mkono au kwa kimombo hand-held magnifiers husaidia baadhi ya watoto. Ikiwa mbinu hii huleta aibu kwao wanapoongeza miaka, angalau jaribu kutathmini kama wao wako tayari kutumia misaada hii kwa ajili ya masomo ya nyumbani. Duka nyingi ambayo hutoa huduma ya kupiga chapa yaweza kuongeza ukubwa wa chapa. Shirika la watu zeru zeru nchini Ghana wanatufahamisha ya kuwa kwa kawaida watu zeru zeru uhitaji maandishi ya herufi ya viwango vya kumi na nane (18) kuwa weshesha kusoma vyema. (Vitabu vingi vya mazoezi huchapishwa kwa viwango vya herufi ukubwa wa kumi na moja (11) ama kumi na mbili (12).

- Kwa waalbino wengi, kuongeza tofauti katika chapa ina faida zaidi kuliko kuongeza ukubwa. Kwa mfano, kwa kutumia kalamu ya rangi nyeusi kwenye karatasi nyeupe ina faida zaidi. Ni rahisi kwa mtoto mwenye ualbino kusoma ubao mweusi kutoka kuliko bao za rangi ya kijani. Ukali wake waweza kuongezwa kwa urahisi sana kwa kuosha ubao kwa maji mara kwa mara. Chaki laini pia huchora mstari bora, na chaki ya rangi-rangi wakati mwingine pia huwa na ufanisi zaidi.

- Kuwaondoa watoto wenye ualbino kutoka darasa za elimu ya michezo au kurekebisha mipango yenu ili kukidhi mahitaji yao. Watoto wenye ualbino wana nguvu za kimwili kama wengine, lakini kama wanatakiwa kufanya shughuli za nje wakiwa wamevaa kaptula au mavazi mengine ambayo huanika ngozi zao kwa jua wakati wa masaa joto ya siku, kutoka saa nne asubuhi mpaka saa kumi alasiri, madhara mabaya yanaweza kusababishwa, ikiwa ni pamoja na kansa ya ngozi. Watoto hawa wanaweza kufanya mazoezi kwenye kivuli au ndani. Kama ni lazima kuwa nje, tafadhali waruhusu kuvaa shati yenye mikono mirefu na suruali ndefu na kofia yenye upana. Hii inaonekana kama kazi nyingi, lakini ushirikiano wenu waweza kumzuia mtoto kutokana na kansa pamoja na kuwapa zawadi ya maisha ya kawaida

- Kumpa ruhusa mtoto kuvaa miwani ya giza wakati yupo nje. Hii ni muhimi ili kimkinga kutokana na madhara zaidi ya jua.

- Tafadhali fanya kila juhidi kuwakinga watoto hawa kutokana na mateso na matusi yanayosababishwa na kutojua. Watoto hawa hawana ugonjya na pia hawana laana. Ni watoto wa kawaida kama wengine na wanahitaji kukubaliwa na jamii na kuwa kama Mungu anavyowataka wawe. Ijapokuwa kuona kwao si kuzuri na ngozi zao nyeti yaweza kudhaniwa kuwa ni ulemavu, wao wanao uwezo wa kuchangia katika kuimarika kwa jamii baada ya marekebisho madogo kufanywa. Matusi hasa haitakiwi kuruhusiwa shuleni. Madhara yake kwa wanafunzi haina kipimo.

- Isipokuwa kwa ajili ya ulinzi maalum kutoka jua na tahadhari maalumu kutokana na kutoona vizuri, watoto waalbino wanapaswa kuchukuliwa kama wengine wote na kuingizwa katika shughuli za shule. Tafadhali hamasisha watoto kuwajumuisha watoto wenye ualbino katika shughuli za kijamii pamoja na kimasomo. Hii ni muhimu sana kwa maendeleo yao.

- Kunaweza kuwa na haja ya kutumia muda katika mkutano shule kuzungumza kuhusu ualbino. Viongozi pamoja na maswali na majibu iliyotayarishwa na Huduma ya Kila Mtoto inapatikana ili kuwasaidia. Baadhi ya mambo ya haja yanayotakiwa kurudiwa tena na tena, kama vile "Ualbino si ugonjwa. Waalbino si watu hatari. Watoto waalbino ni baraka, si laana, ni kama watoto wengine ", na kadhalika.

Kama una maswali yoyote kuhusu ualbino, maafisa wetu wa miradi watafurahi kuzungumza nanyi. Asante kwa michango yenu katika maisha ya watoto na kwa ushirikiano wenu katika masuala haya.

Prepared by Every Child Ministries
Ukurasa umetayarishwa na Huduma ya Kila Mtoto
"Kwa watoto wa Afrika Waliosahaulika"
Barua Pepe : ecmafrica@ecmafrica.org
Maelezo ya Kiswahili na: Lindah Kotut

Every Child Ministries

Maelezo yanayopatikana kutoka kwaHuduma ya Kila Mtoto:

Mafunzo kwa wazazi wa watoto waalbino

Mafunzo kwa watoto waalbino

Maswali na Majibu kuhusu Ualbino

Mapendekezo kwa Walimu katika kuwasaidia watoto wenye Ualbino (waraka huu)

Miwani ya jua na mara kwa mara misaada mengine kwa ajili ya mtoto yeyote aliye na ualbino ambaye anaambatana na mzazi au mlezi na kujisajili katika mojawapo ya ofisi zetu.

ecmuganda@yahoo.com

www.ecmafrica.org

Tembelea wovuti wetu kwa habari ya mara kwa mara.